

**OFISI YA WAKIMBIZI YA JIMBO LA NORTH CAROLINA
MAKUBALIANO YA MAFUNZO YA UJUZI WA UFUNDI NA UTHIBITISHAJI UPYA WA UJUZI
MASHRTI YA MPANGO WA UTEKELEZAJI (DSS-6229)**

Huduma za Msaada wa Wakimbizi za North Carolina zinategemea falsafa ya kujitosheleza na wajibu wa kibinafsi. Hati hii inaelezea hatua zinazohitajika kwa kushiriki katika mafunzo ya ujuzi wa ufundi na uthibitishaji wa ujuzi.

Jina la Mteja: _____ Nambari ya Mgeni: _____

Lengo la Ujuzi wa Ufundi: _____

Lengo la Uthibitishaji wa Ujuzi: _____

Malengo Mengine: _____

Mpango wa Utekelezaji: (Eleza wajibu wa Mteja na/au Shirika)

Mteja/Shirika (C/A)	SHUGHULI/HUDUMA	MATARAJIO	TAREHE INAYOLENGWA	TAREHE YA KUJAZWA

Maoni: _____

Saini zetu zinaonyesha kwamba tumeunda kwa pamoja Mpango huu wa Utekelezaji na tunakubali wajibu na masharti yaliyobainishwa.

_____ Saini ya Mteja

_____ Tarehe

_____ Saini ya Mfanyakazi wa Shirika

_____ Tarehe

_____ Mkalimani

_____ Tarehe

Maagizo ya Kujaza
Fomu ya Makubaliano ya Mafunzo ya Ujuzi wa Ufundi na Uthibitishaji wa Ujuzi wa NC
Mahitaji ya Mpango wa Utekelezaji

Madhumuni: Madhumuni ya **Makubaliano ya Mpango wa Mafunzo ya Ujuzi wa Ufundi (VST) na Uthibitishaji Upya wa Ujuzi (SR)** ni kutoa zana ambayo wafanyakazi wa Mpango wa Msaada wa Wakimbizi na mteja, kwa pamoja, wanaweza kubuni hatua za kuchukua zinazoweza kukamilishwa kwa **Mpango wa Mafunzo ya Ujuzi wa Ufundi na Uthibitishaji Upya wa Ujuzi** na kufanikisha malengo ya mpango wa mafunzo ya ujuzi wa ufundi na/au uthibitishaji upya wa ujuzi. Fomu hiyo inapaswa kujazwa na mfanyakazi/wafanyakazi wa mtoa huduma ya wakimbizi anayehusika na mpango wa huduma za ajira na mafunzo ya lugha ya Kiingereza. Makubaliano ya Mpango wa Mafunzo ya Ujuzi wa Ufundi na Uthibitishaji Upya wa Ujuzi yanapaswa kujumuishwa kwenye faili ya mteja **pamoja na Mpango wa Mafunzo ya Ujuzi wa Ufundi na Uthibitishaji Upya wa Ujuzi wa NC**. Makubaliano hayo LAZIMA yaundwe kwa kila mteja anayepokea mafunzo ya ujuzi na uthibitishaji wa ujuzi.

- Jina la Mteja: Andika jina la mteja binafsi ambaye anaundiwa Mpango wa Utekelezaji na Makubaliano ya Mpango wa Mafunzo ya Ujuzi (VST) na Uthibitishaji wa Ujuzi (SR).
- Nambari ya Mgeni: Weka Nambari ya Mgeni ya mteja.
- Malengo ya Ujuzi wa Ufundi: Eleza kwa ufupi matamano ya mteja ya kupata mafunzo ya ujuzi ambao utamwezesha kupata ajira katika ajira au taaluma maalum.
- Lengo la Uthibitishaji wa Ujuzi: Eleza kwa ufupi matamano ya kuthibitishwa katika taaluma yake ya awali aliyohudumu katika nchi yake ya asili au nje ya Marekani.
- Malengo Mengine: Weka malengo mengine yoyote ambayo mteja anachagua kuyafuatilia yanayohitaji mafunzo na/au uthibitishaji unaomweka kwenye njia ya kupata ajira nzuri.
- Mpango wa Utekelezaji: Jaza chati iliyo hapa chini inayobainisha hatua maalum zinazohitajika kwa mteja na shirika ili kufanikisha malengo ya mafunzo ya ujuzi wa ufundi au lengo la uthibitishaji wa ujuzi.
- C/A: Weka "C" ikiwa shughuli/huduma ni wajibu wa mteja.
Weka "A" ikiwa shughuli ni wajibu wa shirika.
- Shughuli/Huduma: Weka shughuli maalum au huduma inayopaswa kufanywa.
- Matarajio: Weka matokeo yanayotarajiwa ya shughuli au huduma iliyofanywa.
- Tarehe Lengwa: Weka tarehe ambayo shughuli au huduma inapaswa kukamilika.
- Tarehe ya Kukamilishwa: Weka tarehe halisi ambayo shughuli au huduma inakamilishwa.
- Maoni: Weka maoni kuhusu mchakato na mabadiliko au marekebisho yoyote yanayohitajika.
- Saini ya Mteja: Hakikisha mteja anatia saini fomu ya Makubaliano ya Mpango wa Mafunzo ya Ujuzi wa Ufundi/ Uthibitishaji Upya baada ya kufafanuliwa na kutafsiriwa, kama inavyohitajika.
- Tarehe: Weka tarehe ambayo mteja anatia saini fomu ya Makubaliano ya Mpango wa Mafunzo ya Ujuzi wa Ufundi/Uthibitishaji wa Ujuzi.
- Saini ya Mfanyakazi: Hakikisha mfanyakazi anayejaza fomu ya Mpango wa Mafunzo ya Ujuzi wa Ufundi/Uthibitishaji wa Ujuzi anatia saini Makubaliano hayo.
- Tarehe: Weka tarehe ambayo mfanyakazi anatia saini fomu ya Makubaliano ya Mpango wa Mafunzo ya Ujuzi wa Ufundi/Uthibitishaji wa Ujuzi.
- Mkalimani: Hakikisha Mkalimani anatia saini fomu ya Mpango baada ya kufafanuliwa na kutafsiriwa (ikiwa inafaa). Ikiwa hakuna mkalimani aliyehitajika, tafadhali andika N/A (haihusiki).
- Tarehe: Weka tarehe ambayo Mkalimani anatia saini fomu ya Makubaliano ya Mpango wa Mafunzo ya Ujuzi wa Ufundi/Uthibitishaji wa Ujuzi.

Kumbuka: Mfanyakazi wa mtoa huduma anayejaza fomu ya Masharti ya Mpango wa Hatua za Kuchukua wa Makubaliano ya Mafunzo ya Ujuzi wa Ufundi na Uthibitishaji wa Ujuzi anapaswa kuhakikisha mteja anapata nakala iliyotiwa saini ya fomu hiyo baada ya kujazwa.